# Jifunze kusimamia pesa zako nchini Uskoti

Mradi wa kujua kuhusu Pesa

Aprili 2011

FLP - Swahili

**Mradi wa kujua kuhusu Pesa**

Ipindi vyetu vya maelezo vya bure, warsha na kozi hutoa fursa ya kujifunza kuhusu kusimamia pesa zako, kupanga na kujitayarisha kwa maisha yako ya baadaye, na kutatua masuala yoyote unayoweza kuwa nayo ya pesa au hati za madai. Kijitabu hiki kinaonyesha mada zilizoelezwa katika warsha zetu, zinazoonyesha ni nanai anapaswa kuhudhuria na jinsi ya kupata nafasi. Huto maelezo muhimu kuhusu kila ya warsha hizi na huangazia mahali pa kupata ushauri wa kifedha.

**Warsha ni kuhusu nini?**

Warsha zetu huto maelezo kuhusu:

- Benki na akiba,
- bajeti,
- kukopa pesa,
- hati za madai,
- bima,
- kuajiriwa; na
- kuanza biashara yako.

**Ni nani anaweza kuhudhuria warsha hizi?**

Mtu yeyote anaweza kuhudhuria warsha hizi lakini yanafaa sana kwa watu walio na hali Ya Ukimbizi au haki ya kubakia katika Uingereza. Warsha huwa mara kwa mara katika mwaka katika maeneo mengi katika Glasgow. Gharama ya usafiri hulipwa na utunzaji wa watoto unaweza kupatika utakaposema.

Nitapaje kujua zaidi zu kupanga nafasi katika warsha itakayofuata?

Kwa maelezo kuhsu warsha zitakazofuata au kupanga nafasi, tuma barua pepe kwa: financialworkshops@scottishrefugeecouncil.org.uk au rejelea kwa tovuti yetu: http://www.scottishrefugeecouncil.org.uk/how_we_can_help/i_have_refugee_status/leave_to_remain_in_the_uk/financial_literacy_project

Scottish Refugee Council, 5 Cadogan Square, (170 Blythswood Court), Glasgow G2 7PH Tel: 0141 248 9799, Fax: 0141 243 2499,
www.scottishrefugeecouncil.org.uk
Scottish Refugee Council is a charity registered in Scotland.
Registered Charity: SC008639

Maelezo yafuatayo yanaonyesha mada zinazoelezwa kwenye warsha hizi, pia hutoa vidokezo muhimu na maelzo yanayoweza kukusaidia kusimamia pesa zako.

**Benki na akiba**

- Kuna aina nyingi za akaunti za benki na kila lina chaguo na umaarufu wake tofauti. Rejelea kwa kijitabu cha Halmashauri ya Wakimbizi ya Uskoti **'Jinsi ya kufungua akaunti ya benki'** ili kujua mengi kuhusu kufungua akaunti.: http://www.scottishrefugeecouncil.org.uk/assets/0000/0188/How_to_open_a_bank_account_June_2010.pdf
- Aina zingine kwa akaunti za benki ni akaunti za **vyama vya mikopo.** Hizi huwa sawa na benki, na hutumika mitaani na hutoa huduma za ushauri pamoja na huduma za kawaida za kifedha.
- **Fuatilia:** punde unapopata akaunti ya benki au ya chama cha mkopo, ni muhhimu sana kuwa ufuatilie pesa zinaingia na kutoka katika akaunti yako ili kuhakikisha kuwa hutakosa pesa au kupokea gharama za benki kwa kutoa zaidi.

**Kukopa**

- Kuna maeneo tofauti ya njia za kukopa pesa. Unaweza kukopa pesa kwa njia tofauti kama vile mikopo, kadi za mikopo, katalogi, maduka ya kulipia kila wiki au deni la akaunti ya benki. Mara nyingine hili ni kwa sababu ya kulipia bidhaa na mara nyingine ni kupata fedha..
- Gharama ya kukopa pesa kwa njia zilizo hapo juu hulingana. Kwa hivyo ni muhimu sana kuelewa sheria na masharti.
- Unapaswa kulipa riba unapokopa pesa; hii huitwaAPR – **Kiwango cha Asilmia ya Mwaka(APR)**. Kwa jumla jinsi APR ilivyo juu ndivyo pia kiasi cha pesa ambazo unafaa kulipa.
- Unaweza kukosa kukopa pesa iwapo una **kipimo cha chini cha kukopa.** Kipimo cha chini cha mkopo ni utathmini kwa uwezo wako wa kulipa pesa kwa mdaiwa, kama vile benki. Kipimo chako cha ukopaji huamuliwa pamoja na idadi ya mambo kam vile historia yako ya anwani, hali ya ajira, mapato na historia yako ya kulipa madeni..
- Unaweza kuwajibika kutuma ombi la kupat amkopo.  Baadhi ya mikopo inayopatikana ni pamoja na:

- **Mkopo wa uadilifu wa UKBA**
  Mkopo wa uadlifu ni mkopo usio na riba unaotolewa na Ofisi ya Nyumbani ili kuwasaidia wakimbizi. Jua mengi zaidi kwenye tovuti yetu ya Ofisi ya Nyumbani: http://www.ukba.homeoffice.gov.uk/aboutus/workingwithus/workingwithasylum/integration/integrationloan/.

- **Mkopo wa upeo wa tatizo**
  Mkopo huu ni kiasi cha pesa zinazopatikana kutoka kwa Fedha za Jamii ili kukusaidia kununua vyombo vya nyumbani iwapo kuna dharura au msiba. **Utapaswa kulipa pesa hizi baadaye, lakini hakuna riba inayolipishwa**. Hii inamaanisha kuwa unalipa pesa ambazo ulikopa Jua mengi kuhusu mkopo huu, pamoja na mahitaji ya kustahilina jinsi ya kutuma ombi, kwenye tovuti ya Directgov: http://www.direct.gov.uk/en/MoneyTaxAndBenefits/BenefitsTaxCreditsAndOtherSupport/On_a_low_income/DG_10018856

**Hati za madai**

- Iwapo umepokea hali ya ukimbizi au haki ya kubakia katika Uingereza, utawajibika kulipia gharama zako za gesi na stima za kupikia, zakuwasha na kuweka joto nyumbani mwako. Gharama hizi zinaweza kuwa za juu sana na bei yake inaweza kubadilika mwakani. Kwa hivyo unapswa kuangalia gharama hizi ili kuhakikisha kuwa hulipi zaidi au kidogo.

- Nyumba yako lazima iwe na mita, na lazima uisome mita hiyo wakati utakapoingia kwenye nyumba hiyo; unaweza ten akupigia kampuni ya gesi na maelezo hayo. Kusoma mita yako mara kwa mara huhakikisha kuwa unajua ni kiasi kipi cha nishati unachotumia; hii itakusaidia kuelewa hati yako ya madai. Pata ushauri zaidi kuhusu hati zako za gesi na umeme kwenye tovuti ya Wateja ya Consumer Focus Scotland: http://www.consumerfocus.org.uk/scotland/files/2010/11/Tenants-advice-leaflet2.pdf

- Unaweza kulipia mafuta yako kwa njia zingine kadhaa,kwa mfano kwa kulipa katika posta, benki au kwa njia ya maiwa ambapo unatoa idhin kwa pesa kutolewa kwenye akaunti yako kwa wakati fulani uliowekwa. Ni muhimu sana kuwa uweke hati zako na usome mita yako nyumbani, usipofanya hivi, inaweza kuwa rahisi sana kuingia katika madeni na hati zako za madai.

- Jua mengi zaidi kuhusu gharama ya nishati katika Kijitabu cha Halmashauri ya Wakimbizi ya Uskoti ***Mwongozo wa makazi kwa wakimbizi katika Uskoti: Gharama za Nishati*** kinachopatikana kwenye tovuti yetu.: http://www.scottishrefugeecouncil.org.uk/assets/0000/0215/L8_-_fuel_poverty18__Nov_2009.pdf

**Bima**

- Kuna aina nyingi za bima zinazopatikana, kwa mfano, bima ya afya, bima ya afya ya binafs, bima ya vitu vya nyumbani, bima ya ulinzi wa malipo  na bima ya gari.
- Iwapo unaendesha gari **lazima** uwe angalau na bima ya aina ya tatu, lakini aina hizo zingine ni za hiari.
- Mara nyingi mkimu wa makazi yako anaweza kukusaidia kupanga bima ya vitu vya nyumbani kwa bei ya chini. Katika viwango tofauti katika maisha yako itakuwa muhimu kwako kuzingatia ni aina gani za bima zinaweza kufaa kwako na kwa jamii yako.
- Unaweza kununua bma moja kwa moja kutoka kwa kampuni za utaalamu za bima kupitia njia ya simu au tovuti. Unaweza kununua bima pia kutoka kwa benki, maduka makubwa na maduka mengine. Unapswa pia kutafuta bei nzuri zaidi na ulinganishe gharama hizo kwa kutumia tovuti ya ulinganishi kama http://www.gocompare.com/

**Kuanza kazi**

- Utakapoanza kufanya kazi, kutakuwa na mabadiliko katika faida unazopokea. Job Centre Plus na mawakala wengine wa ushauri wa fedha wanaweza kufanya **“Vipimo vya kuwa sawa kazini’,** ili kukusaidia kufanya uamuzi unaofaa kuhusu iwapo uko afadhali ukifanya kazi. Wanaweza pia kukueleza ni fada gani unazostahili kupata. Kuwa katika masomo ya wakato wote pia yataaathiri faida zako. Pata maelezo kuhusu faida kutoka kwa tovuti ya Directgov:  http://www.direct.gov.uk/en/Diol1/DoItOnline/DoItOnlineByCategory/DG_172666
- Unapoanza kazi, unapaswa kupata **karatasi ya maelezo ya malipo**  kila mara, ambayo itaonyesha ni pesa ngapi umepat na makato kutoka kwa malipo yako yote. Kwa kawaida utalipa **ushuru** na **bima ya kitaifa** ; pesa kamili unazolipa hulingana na nambari ya sababu, ikiwa ni pamoja na kiasi unachokadiria kupata mwakani, au iwapo una kazi zaidi ya moja. Jua mengi kuhusu makato na kusimamia pesa zako kwa kutazama video kwenye tovuti ya BBC: http://www.bbc.co.uk/raw/money/new_job/managing_while_you_work.shtml

**Kuanzisha biashara**

- Iwapo ungependa kujiajiri au kuanza biashara yako mwenyewe; kuna mashirika kadhaa ambayo yanaweza kukupa ushauri wa:
    - Business Gateway inaweza kukupa ushauri na maelezo ya kuanza pamoja na usaidizi uliopo kwa biashara zinazoendelea.
      Rejelea kwa tovuti yetu kwa maelezo zaidi: http://www.bgateway.com

- HMRC (Her Majesty's Revenue and Customs) pia wanapatikana kukupa usaidizi kuhusu kutatua masalio ya ushuru.
  Rejelea kwa tovuti ya HMRC kwa maelezo zaidi: www.hmrc.gov.uk

**Ninaweza kupata wapi ushauri zaidi wa kifedha?**

Iwapo utahitaji maelezo zaidi kuhusu kozi hizi na masuala mengine yanayohusika, wasiliana na mfanyakazi katika Halmashauri ya Wakimbizi ya Uskoti : Financialworkshops@scottishrefugeecouncil.org.uk au piga simu kwa 0141 248 9799.

Ushauri wa bure, wa kweli na wa ufaragha unapatikana katika GAIN (Mfumo wa Maelezo na Ushauri wa Glasgow). Rejelea kwa tovuti ya GAIN www.gain4u.org.uk kwa maelezo zaidi kuhusu wakala ulio karibu nawe au simu yao ya usaidizi katika 0808 801 1011.